ipbes
Science and Policy for People and Nature




# Jukwaa la Sera na Sayansi Baina ya Serikali Mbalimbali kuhusu Bioanuwai na Huduma za Mfumo wa Ikolojia (IPBES)

***Taarifa:***

## 'Tathmini ya Mabadiliko ya Mageuzi': Kuzingatia Sababu ya Msingi ya Mgogoro wa Bioanuwai, Vikwazo na Machaguo kwa Ulimwengu wa Haki na Endelevu

## 'Mikakati na Vitendo vya Kuwezesha Upangaji Upya Mkubwa wa Mfumo Mzima'

**Ripoti Imeratibiwa Kuzinduliwa Saa 1pm GMT Jumatano, tarehe 18 Desemba 2024**

*"Tathmini ya Kimataifa ya IPBES iliweka wazi: njia pekee ya kufikia malengo yetu ya pamoja ya maendeleo ni kupitia mageuzi, mabadiliko makubwa ya mfumo mzima kwenye teknolojia, uchumi na jamii. Ili kufanya hivyo, tunahitaji kuelewa vizuri vizuizi, lakini la muhimu zaidi machaguo ya vitendo ambavyo vitaleta ulimwengu wa haki na endelevu zaidi." - Profesa Arun Agrawal, Chuo Kikuu cha Michigan, Mwenyekiti Mwenza wa Ripoti ya IPBES ya tathmini ya Mageuzi*

- **Inaangazia sababu za msingi na athari zake kwa vichocheo vya moja kwa moja vya mgogoro wa bioanuwai**
- **Inatathmini na kulinganisha maono, hali na njia za kufikia ulimwengu wa haki na endelevu zaidi**
- **Inatambua vizuizi muhimu zaidi vya mageuzi**
- **Inatoa mikakati na vitendo vyenye uwezo mkubwa wa kuleta mageuzi na mpito wa haki**
- **Imeandaliwa na wataalamu bingwa 101 kimataifa kutoka nchi 42, kutoka maeneo yote ya ulimwengu**
- **Inatokana na marejeleo 7,000, miaka 3 ikiendelezwa, kwa gharama ya jumla ya zaidi ya dola milioni 1.5**
- **Itaongoza maamuzi na vitendo vya Serikali, asasi za raia, Wenyeji wa Asili na jumuiya za mitaa, biashara na kadhalika ili kufanikisha malengo ya SDG na Maono ya 2050 ya Bioanuwai**
- **Uzinduzi wa Vyombo vya Habari Uliopangwa: 18 Desemba 2024 saa 13:00 GMT/08:00 EDT/14:00 CET/15:00 CAT**
- **Mitandao ya Kijamii: @IPBES #TransformativeChange**

Siku ya Jumatano, tarehe 18 Desemba 2024, Jukwaa la Serikali Mbalimbali la Bioanuwai na Huduma za Mfumo wa Ikolojia (IPBES) linapanga kuzindua **Ripoti yake ya Tathmini kuhusu sababu za msingi za upotezaji wa bioanuwai, viamuzi vya mageuzi na machaguo ya kufanikisha Maono ya 2050 ya Bioanuwai** (inayojulikana kama "Ripoti ya Mageuzi").

**Ripoti hiyo inatathmini viamuzi vya mageuzi, vizuizi vikubwa zaidi ambavyo yanakabili na jinsi yanavyotokea. Pia inatambulisha machaguo yanayoweza kufikiwa ili kukuza, kuharakisha na kudumisha mageuzi kuelekea ulimwengu endelevu na hatua za kufanikisha maono ya kimataifa ya mageuzi.**

Ripoti hiyo **inatarajiwa kujadiliwa na kuidhinishwa katika wiki ya tatu ya Desemba 2024 na Mkutano Mkuu wa IPBES. Mkutano Mkuu unawakilisha karibu Serikali 150** na unajitahidi kuimarisha kiungo cha sayansi na sera kwa ajili ya bioanuwai na huduma za mfumo wa ikolojia.

Ripoti hiyo imekuwa **ikiendelezwa kwa miaka mitatu, kwa gharama ya jumla ya zaidi ya dola milioni 1.5 za Marekani**. Imeandaliwa na **wataalamu bingwa 101 wa kimataifa (ikiwa ni pamoja na Wanazuoni 12) kutoka nchi 42, kutoka maeneo yote ya ulimwengu**, wakiongozwa na wenyekiti wenza watatu: Prof. Arun Agrawal (India na Marekani), Chuo Kikuu cha Michigan; Prof. Lucas Garibaldi (Ajentina), Chuo Kikuu cha Taifa cha Río Negro; na Prof. Karen O'Brien (Norwei/Marekani), Chuo Kikuu cha Oslo. Inatumia takriban marejeleo 7,000 ambayo yanateka uanuwai wa maarifa yaliyopo kuhusu sababu za msingi za upotezaji wa bioanuwai, viamuzi

vya mageuzi na machaguo ya kufanikisha maono ya 2050 ya bioanuwai, pamoja na makala ya kisayansi, ripoti za serikali na bidhaa na mashauriano ya maeneo husika ya maarifa ya Wenyeji wa Asili.

Ripoti hiyo itazingatiwa katika kikao cha kumi na moja cha Mkutano Mkuu wa IPBES (#IPBES11, tarehe 10-16 Desemba 2024). 'Muhtasari kwa Watunga Sera' unaoangazia ujumbe muhimu, matokeo na machaguo **umeratibiwa kuzinduliwa kwa vyombo vya habari vya mseto (ana kwa ana na mtandaoni) huko Windhoek, Namibia, Jumanne, tarehe 17 Desemba 2024 saa 13:00 GMT/14:00 CET/08:00 EST – angalia nyakati nyingine duniani kote hapa:** https://bit.ly/46dvEAZ). **Kiungo cha matangazo ya wavuti ya moja kwa moja: www.ipbes.net**

**Mchakato wa kuvipatia utambulisho vyombo vya habari kwa ajili ya uzinduzi utaanza Oktoba. Ili kupokea mwaliko wa kutambuliwa, waandishi wa habari na mashirika ya vyombo vya habari ambayo bado hayajawekwa kwenye orodha ya vyombo vya habari vya IPBES wanafaa kujisajili hapa: http://eepurl.com/hxkQgn (vyombo vya habari pekee tafadhali).**

IPBES, ambayo mara nyingi huelezewa kama 'IPCC kwa ajili ya Bioanuwai', ni chombo cha kimataifa cha sayansi na sera kilichopewa jukumu la kutoa ushahidi bora unaopatikana kwa watoa maamuzi, kwa ajili ya watu na mazingira ya asili.

### Maswali ya Kujibiwa kwenye Ripoti ya Mageuzi

Ili kuhakikisha umuhimu wa moja kwa moja kwa sera na vitendo vya mageuzi ili kufanikisha Maono ya 2050 ya Bioanuwai, malengo ya SDG na malengo mengine muhimu ya maendeleo ya kimataifa, Ripoti ya Mageuzi inashughulikia maswali mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

- Mageuzi ni nini na yanahusianaje na kusimamia bioanuwai na michango ya mazingira ya asili kwa watu?
- Je, mageuzi yanahusiana vipi na uhusiano kati ya vichocheo visivyo vya moja kwa moja na vya moja kwa moja vya upotezaji na uharibifu wa bioanuwai?
- Vikundi tofauti vina maoni gani kuhusu ulimwengu endelevu na maono haya, na maadili yake ya msingi yanamaanisha nini kwa mabadiliko kwenye sekta mblaimbali na mifumo?
- Ni nini kinachowezesha na kuharakisha mageuzi? Ni vizuizi na changamoto gani zinazozuia mabadiliko hayo na vinawezaje kubadilika baada ya muda, kiwango na muktadha, na vinaweza kushindwaje?
- Watunga sera, wafanya maamuzi, mameneja, wadau, raia, biashara na mashirika yana machaguo na majukumu gani, hayo yanaweza kubadilikaje na jinsi yanavyoweza kufanikishwa

### Muundo wa Ripoti ya Mageuzi

Ripoti ya Mageuzi ina **sura tano**. Sura hizi hutoa msingi wa kisayansi wa ujumbe muhimu wa ripoti. Sura hizo ni:

1. Kuanzisha mageuzi, kuchunguza matokeo ya kutokuchukua hatua na mikakati ya kubatilisha upotezaji wa bioanuwai ndani ya mifumo ya uzalishaji na ulaji
2. Kuunganisha sayansi na maarifa ya asili pamoja na maadili na mitazamo anuwai ya ulimwengu ili kuibua ulimwengu endelevu
3. Kuchambua nadharia, mifumo, kesi za kihistoria, utafiti na vitendo vinavyosababisha mageuzi
4. Kushinda changamoto za kufanikisha mageuzi kuelekea ulimwengu endelevu
5. Kuunganisha mikakati, mbinu, vyombo, machaguo na vitendo kwa ajili ya kufanikisha ulimwengu endelevu kwa ajili ya mazingira na watu

## Matokeo yanayotarajiwa

Ripoti ya Mageuzi ya IPBES:

- Itawapa wafanya maamuzi, pamoja na watunga sera na washika wadau wengi mbalimbali, ushahidi, uchambuzi na machaguo bora yanayopatikana kwa vitendo vinavyoongoza kwenye mageuzi
- Itajenga uelewa wa matokeo ya visababishi vya msingi vya upotezaji wa bioanuwai kwa kufanikisha Mkataba wa Tabianchi wa Paris, malengo ya bioanuwai ya kimataifa chini ya Mfumo wa Bioanuwai wa Kimataifa wa Kunming-Montreal, Malengo ya Maendeleo Endelevu na malengo mengine makubwa ya maendeleo ya kimataifa
- Itachunguza njia za kufikia Maono ya 2050 ya kuishi kwa upatano na mazingira.

## Watathmini na hadhira

Ili kuhakikisha viwango vya juu zaidi vya usahihi, uaminifu na umuhimu wa sera, Ripoti ya Mageuzi ya IPBES imetathminiwa kwa kina kupitia mchakato wa tathmini wa nje ulio wazi, kupitia maelfu ya maoni ya tathmini ya nje, kutoka kwa wanasayansi, wafanya maamuzi (ikijumuisha Serikali), watendaji na wamiliki wa maarifa ya Wenyeji wa Asili na maeneo husika.

Ripoti ya Mageuzi imeandaliwa kwa ajili ya wigo mpana wa wafanya maamuzi, ikijumuisha viongozi wa serikali na biashara, vikundi vya asasi za raia, Wenyeji wa Asili na jumuiya za maeneo husika.

## Podikasti ya IPBES

Ili kusikia zaidi kuhusu wigo huo, ukubwa na umuhimu wa Tathmini hiyo, sikiliza Kipindi cha 4 cha Podikasti ya IPBES, *Nature Insight* – kitakachopatikana kuanzia mwishoni mwa mwezi Novemba 2024 popote unapopata podikasti zako.

| | **RATIBA ya Miaka 3** |
|---|---|
| *Juni 2021* | Mkutano Mkuu wa IPBES, unaojumuisha wawakilishi wa Nchi wanachama wa IPBES, uliidhinisha 'ripoti ya mawanda' inayoanzisha ramani ya tathmini. |
| *Machi 2023* | Wataalam wa nje walitathmini rasimu ya kwanza ya sura, huku maoni ya tathmini yakishughulikiwa katika rasimu zilizofuata na wataalam wa IPBES. |
| *Januari 2024* | Serikali na wataalam walitathmini rasimu ya pili ya sura na rasimu ya kwanza ya muhtasari kwa watunga sera. Maoni haya yameshughulikiwa katika maandishi ya mwisho na wataalam wa IPBES. |
| *Desemba 2024* | Kuzingatiwa kwa maandishi ya mwisho na Nchi wanachama katika kikao cha Mkutano Mkuu wa #IPBES11 ya Muhtasari kwa Watunga Sera mjini Windhoek, Namibia, ikifuatiwa na uzinduzi wa vyombo vya habari uliopangwa kufanyika tarehe 18 Desemba 2024. |

**Ukumbi wa uzinduzi: #IPBES11, Windhoek, Namibia, tarehe 18 Desemba 2024**

**Kwa habari za hivi punde, matangazo ya hivi karibuni, wito kwa wataalamu na kadhalika, jisajili leo kama mshika dau wa IPBES:** www.ipbes.net/stakeholders (mashirika ambayo si vyombo vya habari)

## Kuhusu IPBES

Likiwa na Serikali wanachama karibu 150, Jukwaa la Sayansi na Sera la Serikali Mbalimbali la Bioanuwai na Huduma za Mfumo wa Ikolojia (IPBES) ni chombo cha kimataifa kinachotathmini hali ya bioanuwai na michango ya mazingira ya asili kwa watu, kwa kujibu maombi kutoka kwa wafanya maamuzi na hutoa muhtasari wa machaguo ya siku zijazo kulingana na machaguo tofauti za kijamii na kiuchumi. Dhamira ya IPBES ni kuimarisha sera na maamuzi kupitia sayansi, kwa ajili ya uhifadhi na matumizi endelevu ya bioanuwai, ustawi wa muda mrefu wa binadamu na maendeleo endelevu.

Kamati ya IPBES inaandaliwa na Serikali ya Ujerumani na iko kwenye chuo cha Umoja wa Mataifa huko Bonn. Maelfu kadhaa ya wanasayansi ulimwenguni kote huchangia kazi ya IPBES kwa kujitolea. Wanateuliwa na Serikali au mashirika yao na kuchaguliwa na Jopo la Wataalam wa Taaluma Mbalimbali la IPBES.

*Ripoti ya Tathmini ya Mchavusho ya IPBES, iliyotolewa mwaka 2016, ilikuwa katika lugha 18 na vyombo vya habari zaidi ya 1,300 katika nchi zaidi ya 80. Taarifa ya habari: http://bit.ly/2sq6gbQ*

*Ripoti za Tathmini za Kikanda za IPBES na Ripoti ya Tathmini kuhusu uharibifu na Urejesho wa Ardhi, zilizotolewa mwaka 2017, zilikuwa katika lugha 37 na vyombo vya habari zaidi ya 2,500 katika nchi zaidi ya 124. Taarifa za habari: http://bit.ly/2C0tnNu na http://bit.ly/2ylipyo*

*Ripoti ya Tathmini ya Kimataifa ya IPBES, iliyotolewa mwaka 2019, ilikuwa katika lugha 50 na vyombo vya habari zaidi ya 10,500 katika nchi zaidi ya 170. Taarifa ya habari: http://bit.ly/GlobalAssessment*

*Ripoti za Matumizi Endelevu ya Spishi Mwitu ya IPBES na Tathmini ya Maadili ya IPBES, zilizotolewa mwaka 2022, zilikuwa katika lugha 36 na vyombo vya habari zaidi ya 1,800 katika nchi zaidi ya 100. Taarifa za habari: https://bit.ly/IPBES_SUA na https://bit.ly/IPBES_VA.*

*Ripoti ya Tathmini ya Spishi Vamizi za Kigeni ya IPBES, iliyotolewa mwaka 2023, ilikuwa katika lugha 44, na vyombo vya habari zaidi ya 2,400 katika nchi zaidi ya 105. Toleo jipya: https://bit.ly/InvasiveMedia*

Kwa maelezo zaidi wasiliana na: media@ipbes.net www.ipbes.net

## Fuata IPBES:

x.com/@IPBES
facebook.com/IPBES
youtube.com/ipbeschannel
linkedin.com/company/ipbes
instagram.com/ipbes_
threads.net/@ipbes_
bsky.app/profile/ipbes.bsky.social
mas.to/deck/@ipbes